**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU

# MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI

# HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

---

**21 APRILI, 2026**

# YALIYOMO

*Ukurasa*

**YALIYOMO** .......... **i**
**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... **ii**
**1.0 UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Maelezo ya Awali .......... 1
1.2 Muundo wa Taarifa .......... 2
1.3 Msingi wa Uchambuzi .......... 2
1.4 Mawanda ya Uchambuzi .......... 3
**SEHEMU YA PILI** .......... **3**
**2.0. UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .......... **4**
**2.1 Vipengele vya Uchambuzi** .......... **4**
2.1.2 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Utekelezaji wa vipaumbele hivyo .......... 5
2.1.3 Upatikanaji wa Fedha za Bajeti kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 .......... 6
2.1.4 Fungu Na. 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais .......... 7
2.1.5 Fungu Na. 31 - Ofisi Makamu wa Rais- Muungano .......... 8
**2.2 Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026** .......... **11**
**2.3 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati** .......... **15**
**SEHEMU YA TATU** .......... **15**
**3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** .......... **15**
3.1 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais -Fungu 26 .......... 16
3.2 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)-Fungu 31 .......... 17
**SEHEMU YA NNE** .......... **23**
**4.0 HITIMISHO** .......... **23**

# ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali Na. 1:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 26 .........7

**Jedwali Na. 2:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 31 ......... 9

**Jedwali Na. 3:** Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 Fungu Na. 26............................................. 17

**Jedwali Na. 4:** Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 - Fungu Na. 031 .......................................... 19

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya **Kanuni ya 145** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kugawanyika katika Sehemu kuu Tano kama ifuatavyo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, misingi na muundo wa taarifa hii;
(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuangazia mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;
(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi katika masuala ya Muungano kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
(d) Sehemu ya Nne inahusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na
(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

### 1.3 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi na Maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 unatokana na masharti ya **Kanuni ya 121(4)** ikisomwa kwa pamoja na **vifungu 6(2)(c) na 7 (1)(a)** vya Nyongeza ya

Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni na vifungu hivyo vimeweka masharti yanayoelekeza Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii katika masuala ya Muungano kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

## 1.4 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua jumla ya mafungu mawili (2) ambayo ni: -

a) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; na
b) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira katika masuala ya Muungano.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0. UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 2.1 Vipengele vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 9 na 26 ya mwezi Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira (katika masuala yanayohusu Muungano na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hizo ziliwasilishwa na **Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (Mb),** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hizo umeangazia maeneo makuu manne (4) ambayo ni: -

(a) Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Utekelezaji wa vipaumbele hivyo;

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(c) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kupitia Taarifa ya Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 2.1.2 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Utekelezaji wa vipaumbele hivyo

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Bajeti ulioidhinishwa mwaka 2025/2026. Katika kutekeleza vipaumbele hivyo, Ofisi hiyo inatekeleza majukumu mbalimbali. Baadhi ya majukumu hayo ni kumwezesha Makamu wa Rais kutekeleza ipasavyo jukumu kuu la kikatiba la kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuratibu masuala ya Muungano yapatayo ishirini na mbili (22) kama yalivyoainishwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa vipaumbele hivi. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa kupitia kazi mbalimbali, Wizara imeendelea kutekeleza vipaumbele hivyo kwa ufanisi. Kwa mfano, Kamati ilibaini kuwa Wizara imeendelea kushughulikia na kutatua masuala mbalimbali ambayo awali yalikuwa yanahesabiwa kuwa ni kero kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, na kupelekea idadi ya hoja hizo kupungua kwa kiasi kikubwa. Kutokana

na mafanikio hayo, **Kamati kwa dhati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri wake Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (Mb),** kwa jitihada kubwa wanazoendelea kuzifanya katika kuboresha muungano huu ambao ni mojawapo ya tunu za Taifa.

### 2.1.3 Upatikanaji wa Fedha za Bajeti kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais katika mafungu yake mawili ili idhinishiwa jumla ya shilingi **38,106,589,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Februari, 2026, Ofisi hiyo kwa ujumla wake ilikuwa imepokea shilingi **33,310,479,792.77** sawa na **asilimia 87.41** ya fedha zote zilizoidhinishwa.

Katika kushughulikia bajeti ya Ofisi hii, Kamati imeangazia mapokezi ya fedha hizo fungu kwa fungu katika vipengele vya matumizi ya kawaida ambayo inajumuisha mishahara (PE) na matumizi mengineyo (OC), pamoja na fedha kwa ajili ya maendeleo. Tathmini ya utekelezaji wa bajeti hadi februari, 2026 kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

### 2.1.4 Fungu Na. 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika**; Katika mwaka wa fedha 2025/26 Fungu 26 liliidhinishiwa jumla ya Shilingi **19,946,399,000.00** Kati ya fedha hizo, Shilingi **18,879,500,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **1,066,899,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE).

**Mheshimiwa Spika**; Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026, Fungu 26 limepokea jumla ya kiasi cha shilingi **13,417,088,666.64** sawa na asilimia **67** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi **12,874,666,666.64** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), na shilingi **542,422,000.00** ni kwa ajili ya mishahara. Hali ya mapokezi ya fedha hadi Februari, 2026 inaoneshwa katika **Jedwali Na. 1** kama ifuatavyo: -

**Jedwali Na. 1: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 26**

| MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ZILIZOPOKELEWA | % YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| OC | 18,879,500,000.00 | 12,874,666,666.64 | 68 |
| MISHAHARA | 1,066,899,000.00 | 542,422,000.00 | 51 |
| **JUMLA** | **19,946,399,000.00** | **13,417,088,666** | **67** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa, hadi kufikia Februari 2026 Fungu 26 limepokea jumla ya shilingi **13,417,088,666.64** sawa na **asilimia 67** ya bajeti. Hali hiyo inaonesha kuwa, mapokezi ya fedha kwa Fungu 26 yalizingatia matakwa ya kibajeti kwa, kwani kiwango kinachotakiwa kupokelewa hadi wakati huo ni **asilimia 66.7**.

### 2.1.5 Fungu Na. 31 - Ofisi Makamu wa Rais- Muungano

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Fungu 31 liliidhinishiwa jumla ya Shilingi **18,160,190,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,460,190,000.00** ni za Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 3,115,273,000.00** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **Shilingi 13,344,917,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo iliidhinishwa **Shilingi 1,700,000,000.00**.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu mapokezi ya fedha tathmini inaonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2026 Fungu 31-Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ilipokea jumla ya shilingi **19,893,391,126.13**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **10,973,271,518.00** ni matumizi ya kawaida, sawa na

**asilimia 66.7** ya lengo. Katika fedha za kawaida zilizopokolewa, zinajumuisha mishahara shilingi **2,226,718,600.00** na fedha za matumizi mengineyo shilingi **8,746,552,918.00**. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, zilipokelewa Shilingi **8,920,119,608.13,** sawa na **asilimia 524.7** ya lengo. **Jedwali Na. 2** linaonesha ufafanuzi huo kama ifuatavyo: -

Jedwali Na. 2: **Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 31**

| **Eneo** | **Kiasi Kilichoidhinishwa** | **Kiasi kilichopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Mishahara (PE) | 3,115,273,000 | 2,226,718,600 | 71.47 |
| Matumizi mengineyo-OC | 13,344,917,000 | 8,746,552,918 | 65.54 |
| Jumla Ndogo | 16,460,190,000 | 10,973,271,518 | 66.67 |
| Maendeleo | 1,700,000,000 | 8,920,119,608.13 | 524.71 |
| **Jumla Kuu** | **18,160,190,000** | **19,893,391,126.13** | **109.54** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni wa kutosheleza. Kwa mfano, fedha za maendeleo zilipokelewa kiasi sawa na asilimia **524** ya lengo tarajiwa. Kamati ilielezwa kuwa, kupokelewa kwa kiasi kikubwa zaidi kulitokana na

kupokelewa fedha za ziada shilingi **5,720,119,608.13** kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa Ofisi pamoja na Makazi ya Makamu wa Rais yaliyopo Dodoma na Dar es Salaam. Aidha, shilingi **1,500,000,000.00** zilipokelewa kwa ajili ya uratibu wa shughuli za uchumi wa buluu kufuatia Serikali kuanzisha kitengo hicho, ambacho awali hakikuwepo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kupokelewa kwa fedha za maendeleo kwa asilimia 524 kulizingatia misingi ya kibajeti na ushauri wa Kamati uliotolewa mwezi Aprili, 2025 wakati Kamati ilipowasilisha Maoni yake kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi hii ya Mwaka 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2025/2026.

Kamati katika taarifa yake, ilitoa ushauri kwamba Serikali ihakikishe fedha za maendeleo zilizotengwa zinatolewa kikamilifu ili kukamilisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa, ikiwemo kukamilisha kwa wataki mradi wa ukarabati wa Ofisi za Makamu wa Rais, ili ofisi hizo ziendane na hadhi ya Ofisi hiyo. **Kwa kuwa Serikali imezingatia na kutekeleza ushauri uliotolewa na Kamati kwa wakati, Kamati inatoa pongezi kwa jitihada hizo na kusisitiza kuwa**

**uzingatiaji wa ushauri unaotolewa kwa wakati uwe suala endelevu.**

## 2.2 Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 18 Machi, 2026, Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja unaotekelezwa na Ofisi hii. Mradi huo unahusu Ujenzi wa Jengo la ghorofa sita la Ofisi ya Makamu wa Rais unaotekelezwa katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma (**ambao ni Mradi Namba 6309**).

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa Ofisi hiyo ulianza tarehe 10 Novemba, 2021 ukilenga kukamilika tarehe 9 Novemba, 2023. Hata hivyo, mradi haukukamilika katika muda huo, na hivyo kuongezewa muda hadi tarehe 30 Machi, 2026. Aidha, wakati Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 18 Machi, 2026, ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi wake ulikuwa umefikia **asilimia 94.5**.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa mradi huo unagharimu jumla ya shilingi **24,382,055,160.06**. Katika kiasi hicho, shilingi **22,635,818,859.42** ni kwaajili ya mkandarasi wa ujenzi-SUMA JKT, shilingi **934,693,333.3** ni kwa ajili ya msimamizi wa mradi-Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Shilingi **811,542,967.34** ni kwa ajili ya usanifu wa ujenzi uliotekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

**Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 18 Machi, 2026, jumla ya shilingi **22,998,192,759.66** zilikuwa zimeshatolewa na Serikali na kulipwa kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huu. Katika kiasi hicho, Kampuni ya ujenzi SUMA JKT ilikuwa imeshalipwa shilingi **21,522,001,053.19** sawa na **asilimia 95** ya gharama za mkataba, NHC ilikuwa imeshalipwa shilingi **664,648,739.13** sawa na **asilimia 71** ya gharama za mkataba na TBA ilikuwa imeshalipwa shilingi **811,542,967.34**, sawa na **asilimia 100** ya gharama za mkataba.

Aidha, kuhusu Samani za kuwekwa katika ofisi hizo, Kamati ilielezwa kuwa mkataba wa ununuzi na ufungaji wa samani ulisainiwa tarehe 29 Januari, 2024 kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Kampuni ya *Jaffery Industry Ltd* kwa grahama ya **shilingi 2,114,338,278.** Katika kiasi hicho, ilielezwa kuwa mzabuni ameshalipwa malipo ya awali ya shilingi **845,735,311.00** na ameshakamilisha uwasilishaji wa baadhi ya Samani ambazo zimehifadhiwa ili kusubiria kufungwa mara baada ya ujenzi wa jengo kukamilika. **Kwa kuwa kazi ya ujenzi bado haijakamilika, ni msisitizo wa Kamati kuwa samani zilizokwisha nunuliwa na kuwasilishwa, zitunzwe vizuri ili kuzuia kuharibika uharibifu au kupotea**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokagua mradi huu, ilielezwa kuwa ujenzi wake ulikuwa umefikia **asilimia 94.5**. Licha ya asilimia hiyo, ukaguzi wa Kamati ulibaini kuwa kazi nyingi zilikuwa hazijakamilika kwa asilimia mia moja, jambo lililo ashiria kuwa

bado kuna kazi kubwa ya kumalizia kazi hizo. Kutokana na sababu hiyo, Kamati ilipata wasiwasi kuhusu ujenzi wa jengo hilo kukamilika ifikapo tarehe 30 Machi, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa, sababu za kuchelewa kukamilika kwa mradi huo ni pamoja na mkandarasi kuongezewa muda wa mkataba wa ujenzi, ucheleweshaji wa malipo ya mkandarasi, kuchelewa kwa baadhi ya vifaa vya ujenzi vilivyoagizwa nje ya nchi na kusua sua kwa timu ya ujenzi ya Mkandarasi-SUMA JKT.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutatua changamoto hiyo, Kamati ilielezwa kuwa hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwemo mkandarasi SUMA JKT kubadili timu ya awali iliyokuwa inatekeleza mradi huo (timu kutoka kanda ya kaskazini) na kuleta timu mpya (timu kutoka kanda ya kusini) ambayo ilielezwa kuwa imekuwa ikifanya kazi vizuri.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, licha ya jitihada hizo, miradi ya majengo ya Ofisi inayotekelezwa na Mkandarasi SUMA JKT ikiwemo majengo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria yanayojengwa Mwanza na mji wa Serikali Mtumba-Dodoma hayajakamilika licha ya muda wa utekelezaji kufikia mwisho hata baada ya muda kuongezwa. Aidha, hali ni tofauti kwa miradi kama hiyo inayotekelezwa na Mashirika mengine, hususan miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mji wa Serikali Mtumba.

Kamati inatambua kuwa, ujenzi wa baadhi ya miradi hiyo ilitolewa kwa SUMA JKT ikiaminika kuwa shirika hilo litakamilisha miradi hiyo kwa wakati, hali ambayo imekuwa tofauti. Kutokukamilika kwa jengo hilo kwa wakati, kumesababisha watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kusongamana katika ofisi ndogo ikiwemo kutumia majengo ya kupanga kama ofisi na kumbi za mikutano. Vilevile, kuchelewa huko kumepelekea Ofisi hiyo kutumia jumla ya **shilingi 92,500,000.00** kwa mwaka kwa ajili ya pango la Ofisi na mikutano.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuepukana na hasara na athari hizo, Kamati ilielezwa kuwa, ofisi inaendelea kumsimamia mkandarasi kwa ukaribu ili aweze kukamilisha ujenzi wa jengo hilo na watumishi kuhamia. Aidha, kutokana na matarajio hayo, katika mwaka 2026/2027, fedha kwa ajili ya kukodi pango la Ofisi na kumbi za mikutano kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais zimetengwa **shilingi 10,300,000.00** tu badala ya **shilingi 92,500,000.00** zilizokuwa zikitengwa kwa mwaka. Kufanya hivyo kumeokoa fedha za Serikali kiasi cha **shilingi 82,200,000.00** kwa kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutokuisababishaia Serikali hasara kwa siku za usoni kutokana na baadhi ya miradi inayotekelezwa na SUMA JKT kuchelewa kukamilika kadiri ilivyopangwa, **ni mtazamo wa Kamati kuwa, SUMA JKT ijengewe uwezo ili iweze kukamilisha miradi yote inayokabidhiwa kwa wakati. Aidha, uwezeshaji huo**

**uendane sambamba na kutatua changamoto zinazokwamisha ukamilishaji wa miradi inayokabidhiwa kwa Kampuni hiyo, licha ya washitiri kulipa kwa wakati fedha za kutekeleza miradi hiyo.**

## 2.3 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Baadhi ya mapendekezo ilikuwa ni kutolewa kikamilifu kwa fedha za maendeleo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, tarehe 26 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo katika mafungu yote mawili kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Mafungu hayo ni Fungu 26 linalohusu Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 linalohusu Ofisi ya Makamu wa Rais – katika masuala ya Muungano. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika eneo moja ambalo ni Makadirio ya mapato na matumizi kutokana na Ofisi hii kutokuwa na makusanyo ya maduhuli.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Ofisi ya Makamu wa Rais katika mafungu yake mawili inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **50,465,088,000.00** kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kiasi hicho ni zaidi kwa kiasi cha shilingi **12,358,499,000.00**, sawa na ongezeko la asilimia **32.43** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026 ambayo ilikuwa shilingi **38,106,589,000.00**. Tathmini ya uchambuzi kuhusu fungu kwa fungu ni kama ifuatavyo: -

### 3.1 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais -Fungu 26

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 23,297,959,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,297,959,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na **shillingi 22,000,000,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** kwa ulinganisho kati ya bajeti ya mwaka 2025/2026 na bajeti ya 2026/2027; bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 3,351,560,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 16.80** dhidi ya bajeti ya mwaka unaoisha. Katika ongezeko hilo, Mishahara imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 231,060,000.00** sawa na asilimia **21.66** na bajeti ya Matumizi mengineyo (OC) imeongezeka kwa kiasi cha Shilingi **3,120,500,000.00** sawa na asilimia **16.53**. Mchanganuo huo unaoneshwa katika **jedwali Na. 3** kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 3: **Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 Fungu Na. 26**

| **OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS- FUNGU 26** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | ONGEZEKO | **ASILIMIA** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | OC | 18,879,500,000 | 22,000,000,000 | 3,120,500,000 | **16.53** |
| | MISHAHARA | 1,066,899,000 | 1,297,959,000 | 231,060,000 | **21.66** |
| **JUMLA KUU** | | **19,946,399,000** | **23,297,959,000** | **3,351,560,000** | **16.80** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira na usanifu wa Kamati*

## 3.2 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)-Fungu 31

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, kupitia Fungu 31 katika masuala yanayohusu muungano

inaomba kuidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Shilingi 27,167,129,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **23,467,129,000.00.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kiasi kinachojumuisha mishahara **Shilingi 3,772,212,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 19,694,917,000.00.** Aidha, kiasi kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **Shilingi 3,700,000,000.00** ambazo zote ni fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ulinganisho kati ya bajeti ya mwaka 2025/2026 na bajeti ya 2026/2027, bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa Fungu 31 kwenye masuala ya muungano imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 9,006,939,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 49.6** dhidi ya bajeti ya mwaka unaoisha ambayo ilikuwa **shilingi 18,160,190,000.00**.
Katika ongezeko hilo, Mishahara imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 656,939,000.00** sawa na asilimia **21.09** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha, wakati bajeti ya Matumizi mengineyo (OC) imeongezeka kwa kiasi cha Shilingi **6,350,000,000.00** sawa na asilimia **47.58.** Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa shilingi **2,000,000,000.00** sawa na **asilimia 117.65**. Mchanganuo huo unaoneshwa katika **jedwali Na. 4** kama ifuatavyo:-.

**Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 - Fungu Na. 031**

| OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)- FUNGU 31 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **MAENDELEO** | NDANI | 1,700,000,000 | 3,700,000,000 | 2,000,000,000 | **117.65** |
| | NJE | 0 | 0 | 0 | **-** |
| | **Jumla ndogo** | **1,700,000,000** | **3,700,000,000** | **2,000,000,000** | **117.65** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | OC | 13,344,917,000 | 19,694,917,000 | 6,350,000,000 | **47.58** |
| | MISHAHARA | 3,115,273,000 | 3,772,212,000 | 656,939,000 | **21.09** |
| | **Jumla ndogo** | **16,460,190,000** | **23,467,129,000** | **7,006,939,000** | **42.57** |
| **JUMLA KUU** | | **18,160,190,000** | **27,167,129,000** | **9,006,939,000** | **49.6** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira na usanifu wa Kamati*.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho hapo juu unaonesha kuwa nyongeza kubwa ya fedha imeelekezwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo, ambapo fedha zimeongezwa kwa **asilimia 117.65**. Aidha, fedha zote zilizoongezwa ni fedha za ndani. **Kamati inaipongeza Serikali kwa jithada za kutenga fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa asilimia mia moja. Ni rai ya Kamati kuwa, Ofisi hii iendelee na jitihada hizo katika miaka ijayo**.

## SEHEMU YA NNE

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia majadiliano ya kina na uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo: -

(a) Serikali imeshamlipa mkandarasi anayejenga Ofisi ya Makamu wa Rais katika mji wa Serikali Mtumba kiasi cha fedha sawa na **asilimia 95** ya fedha zote kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi huo. Wakandarasi wengine wanaotekeleza miradi kama hiyo katika eneo hilo wameshakamilisha na kukabidhi kazi hizo licha ya wakandarasi wote kuanza ujenzi wa majengo hayo yanayofanana kwa wakati mmoja. Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais linalojengwa na Kampuni ya SUMA JKT bado halijakamilika, na kutokukamilika huko kunaisababishia Serikali hasara na kuathiri utendaji wa watumishi wa Ofisi hizo. Ili kuhakikisha mkandarasi huyo anatekeleza wajibu wake ipasavyo, Serikali ianze kumtoza fedha za kuchelewesha mradi huo kwa kuzingatia makubaliano yao ya mkataba wa ujenzi.

(b) Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi, idadi kubwa ya Wananachi wa Tanzania wamezaliwa baada ya Muungano wa Tanganyia na Zanzibar uliofanyika mwaka 1964. Kwa kuwa Muungano huo una manufaa mengi na ni moja ya tunu ya Taifa, Kamati inashauri kwamba ili kuendelea kukuza uzalendo wa nchi yetu ikiwemo kulinda, kuheshimu, kupenda na kuenzi Muungano huo, Serikali ihakikishe inaanza ujenzi wa vituo vya Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano katika miji ya

Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar kama ilivyopangwa ili watu waweze kufika kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kujifunza historia ya Muungano huo.

(c) Fedha za bajeti zinazotengwa kila mwaka katika Ofisi ya Makamu wa Rais zimeendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazoukabili Muungano wetu. Aidha, utatuzi huo umekuwa na mafanikio makubwa ambapo kero 22 kati ya kero 25 zimepatiwa ufumbuzi, na hivyo kubakia kero tatu (3) tu. Kamati inashaurii kwamba, ili muungano wetu ufikie kiwango cha kuwa ni jambo la fursa pekee badala ya kuongelea habari za kero, Serikali ihakikishe inazipatia ufumbuzi kero tatu za Muungano zilizobakia na kuzuia kuzaliwa kwa kero nyingine.

(d) Mojawapo ya maeneo mapya ya kiuchumi yanayochipukia nchini ni uchumi wa buluu. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ilianzisha kitengo cha uchumi wa Buluu ili kuweza kuratibu na kuwawezesha wananchi wanaohitaji kujishughulisha na uchumi wa buluu. Katika kuhakikisha wananchi wa pande zote za Muungano wananufaika na uanzishwaji wa kitengo hicho, ni ushauri wa Kamati kwamba Serikali iendelee kukiwezesha kitengo hicho kifedha na rasilimali nyinginezo ili kiweze kuwasaidia

wananchi wa pande zote za Muungano katika kupenda na kuwekeza kwenye uchumi wa buluu.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb | - | **M/Mwenyekiti** |
| 3. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 4. | Mhe. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | - | **Mjumbe** |
| 5. | Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 6. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 7. | Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 8. | Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 9. | Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 10. | Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 11. | Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 12. | Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb | - | **Mjumbe** |
| 13. | Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb. | | **Mjumbe** |
| 14. | Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 15. | Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb | - | **Mjumbe** |
| 16. | Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 17. | Mhe. Dkt. Yahaya Esmail Nawanda, Mb | - | **Mjumbe** |
| 18. | Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 19. | Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 20. | Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb. | - | **Mjumbe** |

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Mhandisi, Hamad Yussuf Masauni, Mb. – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati pamoja na kuwasilisha vizuri

makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Aidha, naomba kumpongeza Mhe. Dkt. Festo Dugange (Mb) aliyekuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano aliokuwa anaipatia Kamati na kwa niaba ya Kamati, ninamtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake mapya ya Naibu Waziri TAMISEMI. Aidha, natumia fursa hii kumpongeza na kumkaribisha Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kamati inamkaribisha na inamtakia kila la kheri katika kazi zake za kumsaidia Waziri wa Nchi  Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara, pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Richard Stanslaus Muyungi, Naibu Katibu Mkuu-Muungano Ndg. Abdallah Hassan Mitawi na Naibu Katibu Mkuu-Mazingira, Balozi Baraka Haran Luvanda.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**

**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

**21 APRILI, 2026**